بسم الله الرحمن الرحيم

## Erdogan Aendelea Kufurahia Uwepo wa Mayahudi

**(Imetafsiriwa)**

**Habari:**

Balozi wa “Israel” jijini Ankara, Irit Lillian, aliwasilisha barua yake ya imani kwa Rais Erdogan. Akiregelea uwasilishaji wa barua ya imani kwa Erdogan kama "wakati wa kihemko", Lillian alisema kwamba anatarajia maendeleo mengi chanya kutokea katika uhusiano kati ya nchi hizo mbili.

Rais wa “Israel” Isaac Herzog, kwa upande mwingine, alishiriki picha za sherehe hiyo ambapo Balozi Lillian alikaribishwa kwa wimbo wa taifa wa “Israel” mjini Beştepe na ujumbe kwa Kituruki kwenye Twitter, ukisema: “Ninatarajia kukubali Barua ya imani ya Balozi wa Uturuki. Hatua kubwa katika mahusiano ya Israel na Uturuki,” alisema. (Mashirika)

**Maoni:**

Pamoja na uamuzi wa "uhalalishaji" uwepo wa gaidi wa Kiyahudi, Uturuki ilianza kuchukua hatua za hila dhidi ya Al-Aqsa mfululizo. Kwanza, kiongozi wa kigaidi Herzog alikaribishwa katika ngazi ya juu zaidi huko Beştepe na tambara la Kiyahudi likabebwa kwa mwanajeshi wa Kituruki. Kisha, mnamo Septemba, Waziri Mkuu wa umbile la Kiyahudi alikaribishwa katika nyumba ya Kituruki jijini New York. Sasa, balozi mpya wa dola hiyo ya kigaidi amewasilisha barua ya imani kwa Erdogan iliyoambatana na wimbo wa taifa "Israel". Kinachofuata ni mapokezi ya Şakir Özkan Torunlar, Balozi aliyeteuliwa na Uturuki kwenda Tel Aviv, na Herzog!

Kwanza kabisa, ifahamike kwamba Waislamu wa Uturuki wamekuwepo tangu maamuzi yote ya khiyana ya Erdogan ambayo yaliwafurahisha Mayahudi. Kwa sababu mtazamo wa Waislamu wa Kituruki kuhusu kadhia ya Palestina sio wa Kimarekani, kama wa Erdogan, wala wa kiakili, wala wa kijinga mno kupendekeza kwamba Palestina itasaidiwa kama rafiki wa “Israel”.

Kinyume chake, mtazamo wa Waislamu wa Uturuki kuhusu kadhia ya Palestina unafanana na mtazamo wa Khalifa Abdul Hamid Khan. Kwa sababu alipoufukuza ujumbe wa Kizayuni kutoka mbele yake, ambao ulitaka kununua ardhi kutoka Palestina kwa kubadilishana na fedha, alisema: “Siwezi kuuza hata shubiri moja ya ardhi nchini Palestina. Kwa sababu ni ya Ummah, si yangu. Ummah huu umeimiliki ardhi hii kwa kutoa damu yao... Mayahudi nawakae na mamilioni yao. Afadhali mwili wangu ukapasuliwa vipande vipande kuliko kutoa shubiri moja ya ardhi kutoka Palestina...”

Mtazamo wa Waislamu wa Kituruki kuhusu kadhia ya Palestina ni kama mtazamo wa kamanda mkuu wa Kiislamu Salahudin, ambaye aliiokoa Al-Qudsi kutoka kwa uvamizi wa Makruseda kwa kuwajibu wale waliosema kwamba kamwe hajawahi kucheka katika hotuba, “Nitawezaje kucheka wakati Al-Qudsi iko chini ya uvamizi?”

Mtazamo wa Waislamu wa Kituruki juu ya kadhia ya Palestina; “Mwenyezi Mungu ametubariki kwa Uislamu. Tukitafuta izza popote pale kando na Uislamu, Mwenyezi Mungu atatushalilisha tena!” kusema hivyo ni kama mtazamo wa Khalifa Omar (ra), mfunguzi wa Al-Qudsi, ambaye alikuwa akitafuta izza na sifa katika Uislamu pekee.

Mtazamo huu kamwe hautabadilika, hautatolewa kafara kwa maslahi yoyote ya mzunguko, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Kwa sababu hiyo ndio kawaida. Kwa hiyo, mapenzi ya Erdogan kwa Mayahudi yatamfunga tu kama fedheha duniani na kosa dhidi yake kesho Akhera. Aidha, hakuwasaliti tu watu wa Palestina pekee; aliwasaliti pia mashahidi wa Mavi Marmara, watoto wa watu wake mwenyewe na Waislamu wa Uturuki, ambao aliwaunga mkono kwa kusema "tukishinda, Al-Qudsi itashinda, Gaza itashinda" kabla ya kila uchaguzi.

Kwa sababu sera ya Uturuki ya Palestina haiongozwi kwa mujibu wa mashtaka ya Ummah, lakini kwa mujibu wa maslahi ya kimataifa ya Amerika. Kama sharti la mkakati mpya wa kisiasa unaolenga kuizingira China na kuidhoofisha Urusi, Marekani inataka matatizo ya Mashariki ya Kati yatatuliwe haraka iwezekanavyo. Kwa kuongeza, ili kusambaza mahitaji ya gesi ya nchi za Ulaya zinazotegemea gesi ya Urusi katika siku zijazo, Uturuki-"Israel" zinahitaji ushirikiano ili gesi asilia ambayo "Israel" imechukua kutoka Palestina kufikia Ulaya. Amerika pia inataka kukengeusha kadhia ya Palestina - katika upinzani wa Palestina na pia katika Ummah - kupitia kuiongeza Uturuki kwenye msafara wa tawala za Kiarabu ambazo zimetia saini khiyana ya "uhalalishaji". Hivyo, anafikiri kwamba kuwepo kwa Mayahudi kutalinda mustakabali wake. Kwa hivyo, lengo pekee la sera ya uhalalishaji ya Erdogan kwa uwepo wa Mayahudi ni kuifurahisha Amerika ili kuendelea kusalia madarakani. Kama vile katika mazungumzo ya uhalalishaji mahusiano yaliyoanzishwa na dhalimu wa Misri na Damascus.

Sisi kama Waislamu, wajibu wetu si kukaa kimya kuhusu usaliti huu wa watawala kwa kugeuza kutazama kwetu kuwa matendo. Ni kuendelea kutetea kadhia ya Palestina, Kibla chetu cha kwanza, bila kuogopa lawama yoyote ya mwenye kulaumu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Wajibu wetu ni kuyakumbusha majeshi ya Ummah juu ya dini, historia na wajibu wao mpaka habari njema ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) itimie na Mayahudi washindwe na Khilafah Rashida irudi Al-Qudsi.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema kama ifuatavyo:

**«لَا تَقُومُ السَّاعَةُ حَتَّى يُقَاتِلَ الْمُسْلِمُونَ الْيَهُودَ فَيَقْتُلُهُمْ الْمُسْلِمُونَ حَتَّى يَخْتَبِئَ الْيَهُودِيُّ مِنْ وَرَاءِ الْحَجَرِ وَالشَّجَرِ فَيَقُولُ الْحَجَرُ أَوْ الشَّجَرُ يَا مُسْلِمُ يَا عَبْدَ اللَّهِ هَذَا يَهُودِيٌّ خَلْفِي فَتَعَالَ فَاقْتُلْهُ إِلَّا الْغَرْقَدَ فَإِنَّهُ مِنْ شَجَرِ الْيَهُودِ»**

**“Kiyama hakitasimama mpaka Waislamu na Mayahudi wapigane. Waislamu watawaua Mayahudi katika vita hivyo (kwa kushinda). Kwa namna ambayo Yahudi atajificha nyuma ya jiwe au mti, na jiwe hilo litasema, 'Ewe Muislamu, ewe mja wa Mwenyezi Mungu! Yahudi huyu hapa nyuma yangu, njoo umuue!'. Isipokuwa tu mti wa Garqad! Kwani ni miongoni mwa miti ya Mayahudi.”** [Muslim, Fiten, 82].

**«فَإِذَا كَانَتْ بِبَيْتِ الْمَقْدِسِ فَثَمَّ عُقْرُ دَارِهَا وَإِنْ يُخْرِجُهَا قَوْمٌ فَتَعُودُ إِلَيْهِمْ أَبَداً»**

**“...kisha Khilafah itarudi tena Bait al-Maqdis wakati huo itakuwa nyumba/mahali ambapo Khilafah itakaa. Hakuna atakayeweza kuitoa humo milele.”**

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**
**Muhammad Emin Yildirim**